**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU,**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA BABATI**

SHULE YA SEKONDARI CHIEF DODO
S.L.P. 288
**BABATI – MANYARA**

Tarehe**…………………**

SIMU NA 0762660485/0693975837
**Kumb Na CDDSS/DED/BBT/JOING INST/KV 2026. /05**

MZAZI/MLEZI WA: ………………………………
S.L.P…………………
……………………….

**YAH: <u>MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI CHIEF DODO DAY ILIYOKO WILAYA YA BABATI MKOA WA MANYARA……………..</u>**

1. **UTANGULIZI**

Ninayo furaha kubwa kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa kuendelea na masomo ya Kidato cha Tano (V) kwa mwaka wa masomo…………kwa tahasusi ya …….., katika shule ya Sekondari Chief Dodo Day.
Muhula wa masomo utaanza tarehe………………….. hivyo Mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe……………………Mwisho **wa kuripoti ni……………………**

Mzazi/mlezi hakikisha unamleta mwanao ili aweze kuandikishwa tarehe iliyotajwa bila kukosa na afike shuleni si zaidi ya saa 10:00 alasiri.

Ni muhimu sana mzazi/mlezi kumsindikiza mwanao hadi hapa shuleni.

**HONGERA SANA!!**

Shule ya Sekondari Chief Dodo Day ipo katika Kijiji cha Riroda Kata ya Riroda, Tarafa ya Gorowa, Wilaya ya Babati, Mkoa wa Manyara. Umbali wa kutoka Makao Makuu ya Mkoa wa Manyara (Babati) hadi Shule ya Chief Dodo ni km 16 kuelekea barabara ya Babati - Singida.

Wanafunzi wanaokuja watashukia stendi kuu ya Babati na kupanda bajaji zinazokuja Riroda mahali ilipo shule kwa nauli ya shilingi 2000/=

***NAKUTAKIA SAFARI NJEMA,***
***KARIBU SANA***

## 2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 2.1. MICHANGO YA KIDATO CHA TANO

| SN | AINA YA MCHANGO | MUHULA 1 |
|---|---|---|
| **01.** | Mchango wa uendeshaji wa Shule | 65,000 |
| **02.** | Nembo | 5,000 |
| **03.** | Tahadhari. | 5,000 |
| **04.** | Kitambulisho | 5,000 |
| | **JUMLA** | **80,000=** |

**Kila mwanafunzi aje na bima yake ya afya (NHIF) ni muhimu sana mwanafunzi hatapokelewa bila kuwa na bima ya afya**.

Michango ya shule ilipwe kupitia akaunti No.**40701200075 NMB** Tawi la Babati Jina la Akaunti ni **Chief Dodo Secondary sc. reccurent. Au Tawi lolote la NMB Tanzania.**

Unatakiwa kuleta Bank pay in slip (BPS) iliyoandikwa jina kamili la mwanafunzi na kidato chake. Siyo jina la mzazi, mlezi.
**ANGALIZO:-*Hatupokei fedha Taslim na fedha zikishawekwa katika akaunti Ya shule hazirejeshwi.***

**2.2. SARE ZA SHULE**: (Mzazi utawajibika kumshonea mwanao sare zote za shule Zinazotakiwa.

2.3 **WAVULANA**

a) Suruali mbili **rangi ya dark blue** zenye mfuko wa nyuma mmoja wenye kuingia ndani, looks 8 yaani mbele nne (kushoto mbili na kulia mbili), nyuma mbili na pembeni mbili. Vile vile iwe na marinda manne (4) celebrations) mbili kila upande chini uweke pindo (turn-up), Suruali za mlegezo, zinazobana (chupa) haziruhusiwi shuleni. Picha imeambatanishwa
b) Unatakiwa kuwa na mashati mawili meupe mikono mirefu aina ya tetroni (cotton) yenye mfuko zinazofaa kufunga tai
c) Soksi jozi mbili rangi nyeusi
d) Sweta rangi moja ya dark blue.
e) Mkanda wa suruali ambao ni mweusi
f) Viatu vyeusi pair 2 vya kufunga na kamba
**g)** Shuka mbili rangi **ya bluu**
h) Suruali ya kushindia rangi ya kijivu.

**2.4. WASICHANA**

a) Sketi mbili rangi ya **dark blue** zenye marinda sita (6) ndefu zinazogusa soksi fupi. Mpangilio wa marinda ni 1 mbele, 1 nyuma, 2 kulia na kushoto- picha imeambatanishwa
b) Unatakiwa kuwa na mashati mawili meupe mikono mirefu aina ya tetroni (cotton) yenye mfuko zinazofaa kufunga tai
c) Soksi jozi mbili rangi nyeupe
d) Viatu jozi mbili rangi nyeusi vya ngozi na vyenye kufunga kwa kamba (gidamu).
**e)** Shuka mbili rangi moja **ya pinki**
f) Sweta mbili **rangi ya dark blue**
g) Shamba dress (gauni la solo) moja lenye rangi ya draft ya damu ya mzee na nyeupe.

2.5. **NGUO NA VIFAA VYA JUMLA**

a) Sweta **rangi ya kijivu kwa ajili ya kushindia**
b) Track suit jozi mbili zenye rangi ya **blue Bahari** yenye michirizi meupe inayoshuka kutoka begani hadi chini
c) Kibanio kimoja cha tai
d) Godoro size 2 ½ x 3x6, mto/foronya 2 zenye rangi inayofanana na shuka
e) Chandarua ya rangi ya bluu.
f) Tochi ndogo kwa ajili ya kutumia wakati umeme wa gridi ukikatika kwa dharura au solata inayotumia mwanga wa jua.
g) Taulo moja, sabuni za kuogea za kutosha, malapa na sabuni ya unga kwa ajili ya kufulia.
h) Sanduku moja imara la bati lenye kufuli **(tranka)**
i) Viatu jozi mbili rangi nyeusi vya ngozi na vyenye kufunga kwa kamba (gidamu)
j) Dawa ya meno, mswaki, na mafuta ya kupata yasiyo na harufu kali. ( aina yeyote ya vipodozi hairuhusiwi )
m) Blanketi kwa ajili ya kujifunika (kuna baridi)
n) T-shirt yenye nembo ya shule inapatikana shuleni kwa bei ya Tsh 15,000/= kwa atakae hitaji kununulia shuleni

2.6. **NGUO ZA MICHEZO**

(i) **Wavulana**

a) Raba jozi moja na njumu nyeusi
b) Bukta moja na T-shirt moja ya njano isiyo na ushabiki wa timu yeyote (yaani isiyo na maandishi) itapatikana shuleni Tsh 18,000/= kwa atakae hitaji kununulia shuleni

(ii) **Wasichana**

a) Raba jozi moja
b) Bukta moja na T-shirt moja ya nyekundu isiyo na ushabiki wa timu yeyote (yaani isiyo na maandishi)

**ANGALIZO**: Uvaaji wa sare ya Shule ni muhimu na ni lazima uwe na sare ya Shule yenye heshima na utakaguliwa ukifika shuleni kama tunavyokuagiza katika fomu hii. Sare ya Shule itatumika wakati wa masomo, ukiwa nje ya shule kwa ruhusa na safarini kuja shuleni na kurudi nyumbani wakati wa likizo.

2.7 **MAAGIZO MENGINE**

1. Madaftari makubwa (counter books quire four) yasiyopungua kumi
2. Kalamu, rula, mkebe na vifaa vya mahesabu (mathematical set), scientific calculators non programmable with the function ranging from fx 82 to fx 991 MS and mathematical table with no formulae na **seti ya Dissecting kit”** na **Dissecting tray** kwa wanafunzi wa CBA.
3. Ndoo mbili za plastic zenye ujazo wa lita 10 moja na ujazo wa lita 20 moja
4. Vitabu binafsi vya masomo kulingana na tahasusi (combination) yako
5. **Ream mbili** (2) za karatasi **A4** kwa mwaka, na rimu moja ruled ( karatasi zenye mistari)
6. File moja kwa ajili ya kuhifadhia nyaraka muhimu.
7. Tai itapatikana shuleni

2.8. **MAVAZI YA KAZI**

- ✓ Suruali mbili (2) GREY ( rangi ya kijivu) **(angalia mshono wa sare ya shule)**
- ✓ Raba nyeusi (mwanafunzi huruhusiwi kuvaa ndala nje ya bweni au darasani ama jikoni)

: 1 Ndala zitatumika ndani ya bweni tu Kwa matumizi ya kuoga
Vazi la kazi litavaliwa na “T-shirt” yenye nembo ya shule.

NB: 2 Mzazi/mlezi utawajibika kumshonea mwanao sare Kama ilivyoelezwa hapo juu
na ajapo shuleni awe amevaa sare ya shule kinyume cha hapo hatapokelewa.

1. **VIFAA VYA USAFI**

   CBA: Aje na jembe 1 yenye mpini ufagio aina ya chelewa, hard broom, ndoo ndogo na ndoo kubwa

   HGK: Aje na, ufagio aina ya chelewa, jembe lenye mpini, squizer, ndoo ndogo na ndoo kubwa na soft broom

**NB:** kila mwanafunzi aje na LITA 3 ya dawa ya usafi.

2. **VYOMBO VYA CHAKULA**
   (i) Aje na sahani ya bati ("Alluminium) moja (1)
   (ii) Aje na bakuli moja (1) bati
   (iii) Aje na kikombe kimoja (1) bati
   (iv) Aje na kijiko kimoja (1)
   NB: Vyombo vya plastic haviruhusiwi kabisa

3. **MAHITAJI BINAFSI YA MWANAFUNZI**

   Mzazi/mlezi unaweza kumpatia mwanao kiasi kidogo cha fedha kulingana na mahitaji yake madogo madogo ya lazima. Haruhusiwi kuja na fedha nyingi na iwapo kuna ulazima wa kumtumia mwanao fedha kwa matumizi yake binafsi tumia njia ya simu ya Makamu/Mkuu wa shule

   **ANGALIZO**: Mzazi/mlezi huruhusiwi kabisa kutumia akaunti ya Shule au mabasi kutuma fedha Kwa ajili ya matumizi binafsi ya mwanao. Pia kuepuka utapeli namba ulizopewa mwanzoni mwa fomu hii zitumike kwa mawasiliano yanayomhusu mwanao pale inapobidi.

4. **MAMBO YA KUZINGATIA WAKATI WA KURIPOTI.**

   Wakati wa usajili mwanafunzi anatakiwa kuwa na nyaraka zifuatazo kwa ajili ya uthibitisho:-
   (i) Sare ya shule (full school uniform) aje akiwa amevaa.
   (ii) Barua yake ya maagizo (joining instruction)
   (iii) Barua ya mzazi/mlezi ya kukubali nafasi hii ikiwa imejazwa kikamilifu (kiambatisho chake)
   (iv) Cheti cha daktari (medical examination form) ambacho kimejazwa vizuri na mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali na siyo Hospitali binafsi. (Kiambatanisho C) .
   (v) Picha nne "passport size" mwanafunzi akiwa katika uniform zake nyuma kitambaa cha blue

**ANGALIZO**

- ✓ Nyaraka zilizotajwa hapo juu ni muhimu sana tafadhali njoo nazo bila kukosa
- ✓ Utasajiliwa ofisi ya Makamu Mkuu wa shule
- ✓ Utawasilisha nyaraka zote za fedha ofisi ya mhasibu
- ✓ Utawasilisha vifaa vyote kama:- Fyekeo,Jembe lenye mpini, ndoo, hard broom, rim pamoja na vifaa vingine katika ofisi ya Mwalimu wa vifaa.

**ONYO!!!**

- ✓ Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo za nyumbani
- ✓ Mwanafunzi haruhusiwi kwenda bwenini kabla ya kukamilisha usajili wake

- ✓ **Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na simu ya mkononi au kitu chochote kinachohusiana na simu, iwapo atakamatwa na simu au kifaa chochote cha**
- ✓ **simu atanyang'anywa na KUFUKUZWA SHULE (hatarejeshewa simu au vifaa hivyo)**
- ✓ Mwanafunzi haruhusiwi kuja na chakula cha aina yoyote ile shuleni
- ✓ Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na pasi ya umeme, heater, kibatari, karabai, mishumaa, radio, camera, television, jiko lolote la kupikia na sufuria, chupa za chai, **NI MARUFUKU**.
- ✓ Mwanafunzi hatakiwi kuchelewa Shule kwa tarehe iliyopangwa na iwapo atachelewa kwa muda wa siku saba (7) baada ya tarehe ya mwisho ya kuripoti bila taarifa ya maandishi atakuwa amepoteza nafasi yake.
- ✓ Mwanafunzi haruhusiwi kufuga kucha, kuweka kucha za bandia, kupaka rangi kwenye kucha, kuweka dawa kwenye nywele, kutumia vipodizi na haruhusiwi kufuga nywele, hivyo atatakiwa kunyoa nywele zake na ziwe fupi muda wote kwa wastani wa kuchana na kutumia kitana kidogo.
- ✓ Mwanafunzi anatakiwa kusoma kuelewa, kuzishika na kuzifuata sheria za Shule ambazo atafafanuliwa mara tu afikapo shuleni. Baadhi ya sheria hizo zimeambatishwa pamoja na form hii.
- ✓ Ni vyema mwanafunzi asindikizwe na mzazi/mlezi wake ili mzazi au mlezi huyo afahamu mazingira ya Shule na mahali shule ilipo na vilevile kufahamiana na watumishi wa Shule na kuwa na uhakika ya kuwa mtoto wake amefika salama mahali panapostahili.
- ✓ Aidha Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na marekebisho yake Na. 10 mwaka 1995 vile vile shule inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini.

Kwa kifupi mwanafunzi azingatie mambo yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa kina mara tu afikapo shuleni.

(i) **Mwanafunzi atatakiwa**

- ✓ Kuheshimu viongozi, wazazi, wafanyakazi wote na jamii kwa ujumla
- ✓ Kuhudhuria vizuri shughuli zote za ndani na nje ya darasa au ya shule
- ✓ Kutekeleza kwa makini na uaminifu na uadilifu mkubwa, shughuli zote za shule kama ilivyo kwenye ratiba.
- ✓ Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine atakazo pangiwa.
- ✓ Kukimbia mara aitwapo na mtu anayemzidi umri.
- ✓ Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo yote juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wake katika shule hii.
- ✓ Kutunza usafi wa mwili na mavazi pamoja na mazingira yote ya shule
- ✓ Kuvaa sare ya shule iliyo safi wakati wote wanapokuwa ndani au nje ya mipaka ya shule, hutakiwi kuvaa mlegezo wala suruali iliyobana.
- ✓ Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote ambapo ratiba ya shule huanza saa 11:00 alfajiri kwasala fupi na mchakamchaka na kuishia saa 4:30usiku baada ya ukaguzi (Bed checking) ambapo taa zote za ndani ya mabweni na madarasa huzimwa na wanafunzi kulala.

**(ii)MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

1. Wizi;
2. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;

3. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
4. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
5. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
6. Kufuga ndevu;
7. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
8. Uvutaji wa sigara;
9. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
10. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
11. Kusababisha mimba;
12. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
13. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
14. **Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;**
15. Kudharau Bendera ya Taifa;
16. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
17. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**Jina la Mkuu wa Shule………………**
**MKUU WA SHULE**

**KIAMBATISHO B**

**OFISI YA WAZIRI MKUU -TAMISEMI**
**SHULE YA SEKONDARI CHIEF DODO**
**FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA SHULE PAMOJA NA MASHARTI YAKE MWAKA 2024/2025**

A. **MWANAFUNZI**

Mimi ……………………………………………nimesoma kwa makini maagizo ya kujiunga na shule ya sekondari ya Chied Dodo Pia nimesoma na kuelewa vyema sheria za shule. Kwa heshima na taadhima na unyenyekevu mkubwa ninakubali/sikubali nafasi hiyo pamoja na masharti na sheria za shule kwa sababu zifuatazo:- (Iwapo unakubali nafasi hii toa sababu vivyo hivyo kama unakataa nafasi toa sababu).

……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
Tarehe …………………………..                         saini …..…………………..

B. **MZAZI/MLEZI**

Mimi……………………………………….mzazi/mlezi wa…………………………………. Ambaye amechaguliwa kujiunga na shule ya sekondari Chief Dodo nimesoma kwa makini maagizo ya shule na sheria zake na kuzielewa vema. Ninakubali/ninakataa nafasi hiyo, ninaahidi/siahidi kumtimizia mtoto wangu mahitaji na maagizo yote ya kujiunga na shule kwa muda uliopangwa. Aidha naahidi/siahidi kushirikiana daima na uongozi wa shule katika kumkuza, kumlea mtoto huyu kwa manufaa yake binafsi, wazazi, jamii na Taifa kwa ujumla.

Kama unakataa eleza sababu:-

……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………

Ahsante

(i) Jina la mzazi/mlezi wa kiume ……………………………………………anwani……………….. Namba ya simu mkononi………………………………… tarehe……………….saini……………

(ii) Jina la mzazi/mlezi wa kike……………………………………… anwani …………………….. Namba ya simu ya mkononi…………………………tarehe………………….saini…………….

Ndugu/jamaa watatu (3) watakaoruhusiwa kumtembelea mtoto/mwanafunzi nje ya wazazi/walezi.

NB **Ndugu na jamaa watakaothibitishwa hawatahusika katika maamuzi ya masuala ya kinidhamu ya mwanafunzi**.

Mimi mzazi/mlezi nathibitisha kuwa waliojiandikisha hapo chini ni ndugu zangu/jamaa wa karibu ambao wanaweza kuruhusiwa kumtembelea mtoto wangu na siyo vinginevyo.

Jina la mzazi/mlezi…………………………………………………saini……………………..

| S/N | JINA MATATU | UHUSIANO WAKE NA MTOTO | ANWANI | SIMU YA MKONONI | SAHIHI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | | |
| 2. | | | | | |
| 3. | | | | | |
| 4. | | | | | |

*Kata lisilohusika*

**NB Sehemu “B” ijazwe na kusainiwa na mzazi/mlezi na si vinginevyo**

**Jina la Mkuu wa Shule……….**

**MKUU WA SHULE**

**KIAMBATISHO C**

**OFISI YA WAZIRI MKUU-TAMISEMI**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**SHULE YA SEKONDARI CHIEF DODO**

**FOMU YA MKATABA WA KUTOSHIRIKI MGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI**

A. **MWANAFUNZI**

Mimi ……………………………………………nimesoma kwa makini maagizo ya kujiunga na shule ya sekondari ya Chief Dodo. Pia nimesoma na kuelewa vyema sheria za shule. Kwa

heshima na taadhima na unyenyekevu mkubwa nathibitisha/sithibitishi kutokushiriki migomo ya aina yoyote, fujo zozote na kosa lolote la jinai katika mazingira hii Chief Dodo Sekondari (Iwapo unakataa mkataba huu toa sababu).

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

Jina........................................................................saini...........................Tarehe.....................

**B. MZAZI/MLEZI**

Mimi……………………………………….mzazi/mlezi wa……………….....………………….

Ambaye amechaguliwa kujiunga na shule ya sekondari Chief Dodo, nimesoma kwa makini maagizo ya shule na sheria zake na kuzielewa vema. Nimekubalina kumshauri mwanangu kutoshiriki katika migomo ya aina yeyote, fujo zozote na jinai lolote awapo katika mazingira ya shule ya sekondari Chief Dodo. Na endapo atakiuka maelekezo yangu haya sheria za shule zichukue mkondo wake.

(Kama unakataa eleza sababu) ………………………………………………….................................

..........................................................................................................................................

Nathibitisha kauli hii mimi Jina .....................................................................................................

mzazi/mlezi wa..............................................................................................................................

saini ...............................................tarehe ...........................................

**KIAMBATISHO D**

**PREME MINISTER OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**CHIEF DODO SECONDARY SCHOOL**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

Ref. No.MBG/ME/VOL. I…....... DATE……………………

To the medical officer
……………………………….
……………………………….
………………………………...
GOVERNMENT HOSPITAL)
STUDENTS NAME…………………………………AGE……………..YEAR………………
Please examine the above name student and arrange for any necessary treatment for student if need be.

**THE HEADMASTER**

Medical certificate
(To be completed by the medical officer)
I have examined the above named with regard to:-

**REMARKS**

1. SKIN ..........................................................................................................................
2. EYES .........................................................................................................................
3. TEETII .........................................................................................................................
4. B/S TEST (CHRONIC) .............................................................................................
5. PRESSURE....................................................................................................................
6. ABDOMEN ...................................................................................................................
7. CHEST .........................................................................................................................
8. STOMACH....................................................................................................................
9. URINE...........................................................................................................................
10. HB.HAEMOGLOBIN.................................................................................................
11. TB TEST.......................................................................................................................
12. VDRI.............................................................................................................................
13. HIV TEST.....................................................................................................................
14. UPT TEST.....................................................................................................................
15. STOOL..........................................................................................................................
16. ULCERS........................................................................................................................
17. DIABETIC.....................................................................................................................
18. ASTHMATIC.................................................................................................................
19. DISABILITIES (If Any)................................................................................................
20. ALLERGIES (If Any) ...................................................................................................
21. ADDITIONAL INFORMATION...................................................................................

Eg.Any physical effects or impartment infections, chronic of family disease etc.

1. The student is in good health free from infection disease and is fit to proceed with studies
2. The student will be attending treatment for ……………………………………………….
   Signature ………………………………………………
   Designation …………………………………………….
   Station …………………………………………………….

NOTE: **MEDICAL OFFICER**

At the time of examination, please treat the individual for any ailment you note

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule …………..**

**Jina la Mkuu wa Shule……………..**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule**

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA**

**UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0762660485**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0783827700**
- **Mwandamizi Taaluma 0674189346**

**VITABU KWA TAHASUSI**

**MWANAFUNZI AHAKIKISHE ANARIPOTI SHULENI NA VITABU VYA MASOMO YAFUATAYO**

- **ACADEMIC COMMUNICATION**
- **HISTORIA YATANZANIA NA MAADILI**
- **GEOGRAPHY**
- **HISTORY**
- **KISWAHILI**
- **CHEMISTRY**
- **BIOLOGY**
- **AGRICULTURE**

Vitabu vyote vizingatie mtaala mpya na viwe vimaendikwa na TAASISI YA ELIMU TANZANIA (TET)

Sare ya wasichana na wavulana

